

# RAIS SAMIA

## aongoza mageuzi ujenzi barabara za lami Tabora

**AZIFUNGUA** barabara za Nyahua - Chaya ya kilometa 85.4, Koga-Mpanda Kilomita 342.9.

**AIPONGEZA** TANROADS, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa kazi kubwa waliyoifanya katika usimamizi wa barabara hizo

Good roads for national development






**BARABARA ya Nyahua hadi Chaya, itarahisisha biashara baina ya Tanzania na nchi za jirani kupitia Bandari ya Dar es Salaam, hivyo kumalizika kwa barabara hiyo ni moja ya mipango bora ya serikali kuwa na miundombinu ya uhakika ya barabara.**

Waziri Profesa Mbarawa

**TANROADS imeitaja barabara ya Tabora-Koga-Mpanda ni moja ya barabara bora zilizojengwa na zinazoendelea kujengwa nchini zenye uwezo kupitisha magari yenye uzito wa tani 65 na ujenzi wake umegharimu sh. bilioni 473.95.**

Eng. Rogatus Mativila

# Rais Samia aifungua barabara ya Nyahua - Chaya ya kilometa 85.4

- **ASEMA** serikali ya awamu ya sita itamaliza na kufungua miradi yote ya barabara nchini
- **APONGEZA** TANROADS kwa kazi bora na ya ufanisi wa ujenzi wa miradi ya barabara
- **ASISITIZA** dhamira yake ni kuifungua nchi kupitia miundombinu ya barabara



NA HAMIS SHIMYE, TABORA

WAKALA ya Barabara Tanzania (TANROADS) imeendelea kudhihirisha kwa vitendo kuwa ni moja ya taasisi bora ya serikali na yenye ufanisi katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (2020-2025), baada ya kuendelea kutafsiri maono ya serikali ya awamu ya sita kwa kuleta maendeleo nchini.

Hali hiyo inatokana na TANROADS kusimamia kwa ukamilifu ujenzi wa barabara ya Nyahua- Chaya yenye urefu wa kilometa 85.4 iliyojengwa kwa kiwango cha lami na Rais Samia Suluhu Hassan, kuifungua rasmi. Barabara hiyo ni sehemu ya barabara ya Tabora-Nyahua-Chaya yenye urefu wa kilometa 170.

Ufunguzi wa barabara hiyo, ulifanywa na Rais Samia Mei 17, 2022, eneo la stendi ya mabasi ya Tura lililoko wilayani Uyui mkoani Tabora, ambapo Rais anasema ufunguzi wa barabara hiyo ni kielelezo tosha kuwa serikali ya awamu ya sita imedhamiria kwa dhati kuifungua nchi kwa miundombinu ya barabara.

Barabara ya Tabora-Nyahua-Chaya, sehemu ya Nyahua-Chaya yenye urefu wa kilometa 85.4, imejengwa kwa sh. bilioni 123.9 ikiwa ni mkopo wenye masharti nafuu kutoka Mfuko wa Maendeleo ya Kiuchumi ya Kuwait (KFAED), ambapo Tanzania imechangia asilimia 28 na KFAED imechangia asilimia 72 katika mkopo huo.

Anasema kukamilika kwa barabara hiyo kutapunguza urefu wa safari kwa magari yanayopita katika barabara hiyo na kuleta tija kwa wasafiri na wasafirishaji wa mikoa ya Tabora, Kigoma na Katavi, ambao wamekuwa wakipitisha bidhaa zao.

Rais Samia anasema serikali itahakikisha inamaliza na kufungua miradi yote ya barabara iliyomalizika kujengwa nchi nzima kwa kuwa nia na dhamira yake ni kuhakikisha anaifungua nchi kupitia miundombinu ya barabara ili wananchi waweze kufanya shughuli zao kwa ufanisi mkubwa.

"Ufunguzi wa barabara hii ni moja ya miradi ambayo serikali ya awamu ya sita imeietekeleza. Natambua kuna miradi mingi ya barabara imemalizika na inasubiri kufunguliwa katika mikoa ya Njombe, Mtwara na kwingineko. Nawaahidi nitaifungua kwa kuwa Serikali imedhamiria kuifungua nchi kupitia barabara," anasema.

Anaongeza: "Naipongeza TANROADS, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa kazi kubwa waliyoifanya katika usimamizi wa barabara hiyo iliyotengenezwa na Kampuni ya China Henan International (CHICO) kwa kiwango cha lami kwa ufanisi mkubwa."

Rais Samia anasema amedhamiria kuufanya mkoa wa Tabora kuwa na barabara za lami kwa kuwa anapofungua barabara hiyo anajiwa na historia kubwa kuhusu mkoa huo

Barabara ya Tabora-Nyahua-Chaya, sehemu ya Nyahua-Chaya yenye urefu wa kilometa 85.4, imejengwa kwa sh. bilioni 123.9 ikiwa ni mkopo wenye masharti nafuu kutoka Mfuko wa Maendeleo ya Kiuchumi ya Kuwait (KFAED), ambapo Tanzania imechangia asilimia 28 na KFAED imechangia asilimia 72 katika mkopo huo. Kukamilika kwa barabara hiyo kutapunguza urefu wa safari kwa magari yanayopita katika barabara hiyo na kuleta tija kwa wasafiri na wasafirishaji wa mikoa ya Tabora, Kigoma na Katavi, ambao wamekuwa wakipitisha bidhaa zao.

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa





# Barabara ya Nyahua hadi Chaya yafunguliwa rasmi

katika kichwa chake, historia aliyoipata akiwa bungeni kutoka kwa Mbunge wa Urambo, Magreth Sitta.

Anasema wakati akiwa mbunge ndani ya Bunge, Mbunge wa Urambo, Magreth alikuwa analalamika ukosefu wa barabara za lami mkoani humo, licha ya mkoa huo kuwa chachu ya kupigania Uhuru wa Tanzania, ambapo sasa anamuhakikisha kuwa mkoa huo utakuwa na barabara za lami.

"Nafarijika sana ninapofungua barabara hii, nakumbuka dada yangu Mama Sitta aliwahi kulalamika bungeni. Sasa namwambia serikali ya awamu ya sita italimaliza hilo na kuhakikisha mkoa mzima unakuwa na barabara za lami ili kurahisisha shughuli za usafiri na usafirishaji kufanyika kwa kasi," anasema.

Anaongeza "Barabara hii ni muhimu sana kwa kuwa ni barabara kuu inayounganisha Tabora na mikoa mingine ikiwemo Singida, Kigoma, Katavi na nchi jirani za DRC na Burundi. Hivyo kumalizika kwa kipande hicho ni fursa kubwa ya kiuchumi kwa nchi," anasema.

Anasema barabara hiyo pia itarahisisha biashara baina ya Tanzania na nchi za jirani kupitia Bandari ya Dar es Salaam, hivyo



**Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa amewataka wakazi wa mikoa ya Tabora, Kigoma na Katavi kuitumia barabara hiyo kujiletea maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa kuwa ujenzi wa barabara hiyo ni nyenzo kwao kujikomboa.**

kumalizika kwa barabara hiyo ni moja ya mipango bora ya serikali kuwa na miundombinu ya uhakika ya barabara.

"Nawashukuru sana Mfuko wa Kiuchumi wa Maendeleo wa Kuwait kwa kufanikisha ujenzi wa barabara hii, hivyo naahidi ushirikiano wa dhati na nchi ya Kuwait na Tanzania kuendelea kwa kuwa ni marafiki wa muda mrefu na serikali itaendelea kudumisha uhusiano huo na umoja uliopo," anasema.

Anasema Serikali inaendelea na ujenzi wa barabara na madaraja ili kuifungua na kuunganisha nchi katika kanda zote na hivyo, kuchochea maendeleo kwa kasi kwa wananchi, hivyo wananchi wana wajibu wa kuitunza barabara hiyo na miundombinu yake.

"Barabara zinajengwa kwa fedha nyingi hivyo zitunzeni ili zidumu kwa muda mrefu na zitumieni kukuza shughuli za kiuchumi. Kuna tabia za baadhi ya watu kuhujumu miundombinu, hivyo wanapaswa kutambua kuwa serikali itawachukulia hatua kali wanaoendekeza vitendo hivyo," anasema.

Anaongeza: "Acheni kuchimba mchanga kwenye hifadhi za barabara na madaraja kwani kufanya hivyo ni kuhujumu miundombinu na kuisababishia Serikali hasara na kero kwa wananchi."

### WAZIRI PROFESA MBARAWA AWATAKA WANANCHI KUITUMIA BARABARA HIYO KUKUZA UCHUMI

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa, amewataka wakazi wa mikoa ya Tabora, Kigoma na Katavi kuitumia barabara hiyo kujiletea maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa kuwa ujenzi wa barabara hiyo ni nyenzo kwao kujikomboa.

Anasema Wizara itaendelea kuiimarisha Bodi ya Mfuko wa Barabara ili uhudumie barabara nyingi zaidi na kumalizika kwa barabara hiyo ni moja ya juhudi ya Rais Samia kuhakikisha nchi inakuwa na barabara za lami zenye viwango vya juu ili kuwarahisishia wananchi maendeleo.

Waziri Profesa Mbarawa anasema ujenzi wa barabara hiyo ni sehemu ya mikakati ya serikali ya awamu ya sita kuhakikisha wanatekeleza miradi yote iliyopo kwa kuhakikisha inamalizika kwa wakati na kwa ubora unaotakiwa, hivyo wananchi wanapaswa kuunga mkono juhudi hiyo kwa kutunza, kulinda miundombinu ya barabara. "Tunakupongeza Rais Samia kwa juhudi zako za kuhakikisha kila siku miradi ya barabara inajengwa na kumalizika ili kuifungua nchi, hivyo nikiwa kama Waziri nitahakikisha nazitaka taasisi zote zilizo chini yangu kuhakikisha zinamaliza miundombinu wanayoisimamia," anasema.

### BUNGE LAMPONGEZA RAIS SAMIA KWA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA BARABARA

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Moshi Kakoso, anasema amekuwa akipita maeneo mbalimbali ya

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa

# Rais Samia aifungua barabara ya Nyahua



nchi na kushuhudia mafanikio makubwa ya serikali ya awamu ya sita katika kutekeleza miradi ya miundombinu kwa kasi kubwa.

"Wanaosema hakuna miradi inayoendelea nchini wanadanganya na wanapaswa kukemewa, Rais Samia unafanya kazi kubwa ya ujenzi wa miradi ya miundombinu na hilo sisi kama Bunge tumeliona katika ziara zetu tunazofanya maeneo mbalimbali ya nchi," anasema.

Anasema ujenzi wa barabara hiyo ni kielelezo tosha kuwa serikali ya awamu ya sita imedhamiria kuwakomboa wananchi kiuchumi kwa kuwa barabara hiyo ni msaada kwa wakazi wa Uyui na mkoa mzima wa Tabora kwa kuwa itawasaidia kusafirisha bidhaa zao kutoka Tabora na kwenda mikoa mingine.

"Ufunguzi wa barabara hiyo una manufaa makubwa kwa nchi, kwa kuwa barabara hiyo ni muhimu katika kuiunganisha nchi na nchi za jirani katika ufanyaji wa biashara. Tunakupongeza wewe binafsi na serikali kwa kazi kubwa ya kuwaletea maendeleo wananchi," anasema.

"Wanaosema hakuna miradi inayoendelea nchini wanadanganya na wanapaswa kukemewa, Rais Samia unafanya kazi kubwa ya ujenzi wa miradi ya miundombinu na hilo sisi kama Bunge tumeliona katika ziara zetu tunazofanya maeneo mbalimbali ya nchi," anasema. Anasema ujenzi wa barabara hiyo ni kielelezo tosha kuwa serikali ya awamu ya sita imedhamiria kuwakomboa wananchi kiuchumi kwa kuwa barabara hiyo ni msaada kwa wakazi wa Uyui na mkoa mzima wa Tabora kwa kuwa itawasaidia kusafirisha bidhaa zao kutoka Tabora na kwenda mikoa mingine.

**Rais Samia ameweza kutatua kero na shida za wananchi kupitia fedha za Uviko-19, ambapo mkoa huo umebahatika kutekeleza miradi mingi ikiwemo ujenzi wa shule shikizi, madarasa, vituo vya afya na mambo mengine mengi.**

**DKT. BATILDA**



**KUWAIT YAAHIDI USHIRIKIANO NA TANZANIA**

Naibu Mkurugenzi Mkuu wa KFAED, Waleed SH. Albahar, alimpongeza Rais Samia kwa uongozi wake na kumuahidi Kuwait itaendelea kushirikiana na Tanzania katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kimaendeleo nchini kwa kuwa imekuwa ikishirikiana kwa muda mrefu.

"Umekuwa ukifanya kazi kubwa ya ujenzi ya miundombinu, Tutaendeleza ushirikiano huu ambao umedumu kwa muda mrefu na tuna matumaini makubwa ushirikiano huu utaendelea zaidi kwa kuwa Tanzania na Kuwait wamekuwa marafiki toka 1978," anasema.

Anaongeza: "Tunapongeza ushirikiano baina ya Wizara ya Fedha na Mfuko wa Kuwait, watu wote walioshiriki ujenzi wa mradi huu wa barabara, ambao una manufaa makubwa kwa wananchi na serikali ya Tanzania katika kuwaletea maendeleo," anasema.

**DKT. BATILDA ASEMA BARABARA HIYO INAUFUNGUA KIUCHUMI MKOA WA TABORA**

Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Balozi Dkt. Batilda Burian, anasema anampongeza Rais Samia kwa kuupiga mwingi na katika kipindi chake cha mwaka mmoja, amekuwa kiongozi aliyeleta mafanikio makubwa mkoani humo, ikiwemo utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimaendeleo.

Anasema Rais Samia ameweza kutatua kero na shida za wananchi kupitia fedha za Uviko-19, ambapo mkoa huo umebahatika kutekeleza miradi mingi, ikiwemo ujenzi wa shule shikizi, madarasa, vituo vya afya na mambo mengine mengi.

"Sisi tumesema Tabora wao ni Nyuki wa Mama, hivyo tutakulinda kwa nguvu zote kwa kuwa uwepo wa miradi mikubwa ya kimaendeleo



# Rais Samia aifungua barabara ya Nyahua



hususan ya ujenzi mkoani kwetu ni chachu ya maendeleo kwa mkoa na nchi kwa ujumla. Tunakushukuru sana Rais Samia," anasema.

Balozi Dkt. Batilda anasema akiwa Mkuu wa Mkoa huo, atahakikisha barabara hiyo inalindwa kwa kuwa imekuwa msaada kwao katika kuleta maendeleo kwa wananchi kwa kuwa imerahisisha usafiri kwa wananchi kutoka Singida, Tabora, Katavi hadi Kigoma.

**WABUNGE WAISHUKURU SERIKALI**

Wabunge wa majimbo yanayounda wilaya ya Uyui, mkoa wa Tabora, Igalula na Tabora Kaskazini (Uyui), wamesema ujenzi wa barabara hiyo ni kielelezo tosha kuwa serikali ya awamu ya sita imekuwa mstari wa mbele katika kuwatumikia wananchi katika ujenzi wa miundombinu.

Mbunge wa Igalula, Venance Protas, anasema akiwa mbunge wa eneo hilo, ambapo barabara hiyo imepita anaishukuru serikali na Rais Samia kwa kuwa wamemrahisishia kazi kwa wananchi na ujenzi huo umetekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

"Tunakushukuru sana Rais Samia umetupa heshima kubwa kwa ujenzi wa barabara hii. Umekuwa na nia ya dhati ya kuleta maendeleo nchini. Nimesimama kukueleza asante na tutazidi kukupenda daima," anasema Mbunge huyo huku akiongeza barabara hiyo imekuwa msaada mkubwa kwao.

Anasema serikali ya awamu ya sita imekuwa ikitekeleza miradi mingi ya ujenzii katika jimbo la Igalula, ikiwemo mradi wa reli ya kisasa ya SGR, hivyo kumalizika kwa mradi huo wa barabara ni faraja kubwa kwao na utazidi kuwanufaisha wananchi wa eneo hilo kiuchumi.

Naye, Mbunge wa Tabora Kaskazini (Uyui), Almas Maige, anasema Wilaya ya Uyui ina majimbo mawili, ambayo ni Igalula na Tabora Kaskazini, anampongeza Rais Samia kwa kufungua barabara hiyo kwa kuwa amefanya kitu kitakachoachа historia kubwa kwao juu ya barabara hiyo.

Naye, Kashinde Abdulrahman ambaye ni mkazi wa Igalula ,anasema yeye binafsi anamuona Rais Samia kama malkia aliyekuja kuwakomboa Tabora kwa kuwa ameweza

**Mbunge wa Igalula, Venanc Protas, anasema akiwa kama mbunge wa eneo hilo ambapo barabara hiyo imepita anaishukuru serikali na Rais Samia kwa kuwa wamemrahisishia kazi kwa wananchi na ujenzi huo umetekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM. "Tunakushukuru sana Rais Samia umetupa heshima kubwa kwa ujenzi wa barabara hii. Umekuwa na nia ya dhati ya kuleta maendeleo nchini. Nimesimama kwa kukueleza asante na tutazidi kukupenda daima...**

kubadilisha hali na maisha ya vijana, ambao wengi walikuwa hawana shughuli za kufanya, lakini ujio wa miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa barabara hiyo iliyomalizika na ujenzi wa reli ya kisasa ya Stardand Gauge ni fursa adhimu.

"Kaka, nakuambia vijana wengi sasa wako katika ujenzi wa reli wanafanya kazi za vibarua na uhakika wa kupata elfu 10 ni mkubwa, maisha ya vijijini ni magumu na inapotokea miradi kama hii ndio fursa yenyewe. Tunamshukuru sana kwa kuwa amekuwa akifanya kazi kubwa," anasema.

Kashinde anasema akiona barabara nzuri ana kumbuka mambo mengi, ambapo zamani walikuwa wanatumia hadi saa nne au tano kufika Tabora mjini, lakini sasa hali imekuwa tofauti kutokana na uwepo wa barabara iliyojengwa kwa kiwango cha lami.

"Kipindi cha masika ndugu yangu, hali ilikuwa mbaya sana, hususan katika daraja la Kizengi na Nyahua, ambapo kulikuwa kuna sababisha adha kubwa ya usafiri na hata watu wakati mwingine kupata matatizo ya kiuchumi, ikiwemo kushindwa kusafirisha mizigo yao kupeleka Tabora, Mpanda au Singida," anasema.

Hivyo, ataendelea kumshukuru Rais Samia na TANROADS kwa kazi kubwa waliyoifanya ya ujenzi wa barabara hiyo, ambayo kwao imekuwa mkombozi mkubwa kwa kuwa walikuwa wanaishi katika mateso makubwa kutokana na kukosa kwa miundombinu bora ya barabara.

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa



# Fahamu ubora, upekee wa barabara ya Nyahua-Chaya

- **ENG.** Mativila ampongeza Rais Samia kwa kuwaondolea adha wananchi
- **BARABARA** ya Manyoni-Itigi-Tabora kuwa ya kisasa ya kiwango cha lami

Na Mwandishi Wetu



MRADI wa ujenzi wa barabara ya Nyahua-Chaya yenye urefu wa kilometa 85.4 unaelezwa kuwa moja ya miradi bora ya barabara inayoendelea kujengwa nchi nzima na serikali ya awamu ya sita chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Mradi huo ni sehemu ya barabara ya Manyoni mkoani Singida hadi Tabora yenye urefu wa kilometa 259.7, ambayo serikali ya awamu ya sita imeutekeleza ikiwa na lengo la kuhakikisha ukanda wa kati (central corridor) kuna kuwa na barabara nzuri za lami.

Sehemu ya Barabara ya Nyahua hadi Chaya imejengwa kwa gharama ya sh. bilioni 123.9, ikiwa imegharamiwa ni mkopo wa gharama nafuu kutoka Mfuko wa Maendeleo ya Kiuchumi ya Kuwait (KFED), ambapo Tanzania imegharamia kwa asilimia 28 huku Kuwait ikigharamia kwa asilimia 72.

Akiuzungumzia mradi huo, Mtendaji Mkuu Wakala ya Barabara nchini (TANROADS), Eng. Rogatus Mativila, anasema ujenzi wa barabara ya Nyahua-Chaya umehusisha madaraja makubwa mawili, makalvati makubwa 32 na madogo 60.

Anasema ufunguzi wa barabara hiyo ni sehemu ya mradi wa ujenzi wa barabara kuu ya Tabora-Nyahua-Chaya yenye urefu wa kilometa 170 kwa kiwango cha lami uliokuwa unatekelezwa na serikali kwa usimamizi wa TANROADS, ikiwa ni moja ya mipango ya serikali katika ujenzi wa miundombinu ya barabara.

"Mheshimiwa Rais, sehemu ya mradi wa barabara hiyo Nyahua-Chaya yenye kilometa 85.4, ambayo utaifungua ni sehemu ya barabara kuu iliyoanzia Manyoni hadi Tabora yenye urefu wa kilometa 259.7. Barabara hii inaunganisha ukanda wa kati kuanzia Manyoni na kupitia mikoa ya Tabora, Kigoma na Katavi," anasema.

Eng. Mativila anasema pia barabara hiyo inaunganisha Bandari ya Dar es Salaam na nchi za Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC) na Burundi kwa kupitia Bandari ya Kigoma na Karema, hivyo ujenzi wa barabara hii ni moja ya fursa kubwa kiuchumi kwa Tanzania kuendelea kuhudumia shehena za mizigo na abiria.

**"Kukamilika kwa barabara hii sasa kunaifanya barabara yote ya Manyoni-Itigi-Tabora kuwa ya kiwango cha lami na hivyo kupunguza msongamano kwenye barabara ya Nzega-Singida-Manyoni, ambayo watu walikuwa wanapita huko kutokana na uchakavu wa barabara uliokuwepo awali" anasema. Anaishukuru serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Samia kuendelea kuiamini TANROADS kwa ...**

**USANIFU WA MRADI**

Eng. Mativila anasema upembuzi yakinifu na usanifu wa barabara hiyo kutoka Tabora-Nyahua-Chaya yenye urefu wa kilometa 170 ulifanywa na kampuni ya Crown Teck-Consult Ltd ya Tanzania kwa gharama ya sh. bilioni 1,374,980,000.00 na kazi ilikamilika Mei 2011.

Anasema mapitio ya usanifu wa kina na uandaaji wa nyaraka za zabuni ulifanywa na kampuni ya Engineering Consultant Group (ECG) ya Misri ikishirikiana na Kampuni kutoka Kuwait ya Industrial and Engineering Office pamoja na Tanzania Building Agency (TBA) kwa gharama ya sh. bilioni 703,456,435.56 na kazi hiyo kukamilika Septemba, 2016.

Anasema kulingana na usanifu wake, barabara hiyo imejengwa kwa upana wa mita 9.5, ambapo mita 6.5 ni njia ya magari na mita 1.5 kila upande ni mabega ya barabara kwa ajili ya watembea kwa miguu na kuipa uwezo na uimara barabara hiyo kupitisha watu na magari bila wasiwasi wowote.

"Matabaka ya chini ya barabara hiyo yaani G7 na G15 yote yamejengwa kwa unene wa milimita 150. Huku tabaka la msingi lina unene wa milimita 200, ambapo limejengwa kwa kuchanganya changarawe na saruji (cement stabilized subbase (C1) )," anasema Eng. Mativila.

Anasema pia tabaka la kati (CRR Base Course) lina unene wa milimita 150 na limejengwa kwa mawe yaliyosagwa na tabaka la juu (Wearing Course) limejengwa kwa lami nyepesi (Double Surface Dressing) na kuifanya barabara hiyo kuwa imara na yenye uwezo wa kudumu kwa miaka mingi zaidi.

"Uwepo wa madaraja yaliyojengwa imara yanaongeza uimara wa barabara hiyo, ambayo ina madaraja mawili yenye urefu wa 68 kila moja kwa sehemu ya Nyahua na Kizengi, pia kuna makalavati makubwa 'box culvert' 32 na makalavati madogo 60, ambayo nayo yamejengwa katika barabara hiyo," anasema.

Kwa mujibu wa Eng. Mativila, mradi huo umejengwa na kampuni ya China Henan International Cooperations (CHICO) ya China kwa gharama ya sh. bilioni 123,916,039,542.98 ikijumuisha kodi ya ongezeko la thamani yaani VAT ikiwa ni gharama ya ujenzi wa barabara hii.

Aidha, anasema mhandisi mshauri wa mradi huo alikuwa kampuni ya Abduljebain Engineering Consulting Office ya kutoka Kuwait, ambapo walishirikiana na kampuni ya DOCH Ltd ya Tanzania katika ushauri wa ujenzi wa barabara hiyo ya Nyahua-Chaya yenye urefu wa kilometa 85.4.

"Kukamilika kwa barabara hii sasa kunaifanya barabara yote ya Manyoni-Itigi-Tabora kuwa ya kiwango cha lami na hivyo kupunguza msongamano kwenye barabara ya Nzega-Singida-Manyoni, ambayo watu walikuwa wanapita huko kutokana na uchakavu wa barabara uliokuwepo awali," anasema.

Anasema anaishukuru serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Samia kuendelea kuiamini TANROADS kwa kuipa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ya ujenzi wa barabara, madaraja na viwanja vya ndege kwa ufanisi mkubwa.

"Tunachokuahidi ni kutokuangusha kwa kuwa tumedhamiria kufanya kazi kubwa ya kuhakikisha tunatekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa ufanisi mkubwa kwa kuwa wajibu wetu ni kuhakikisha dira na maono makubwa uliyokuwa nayo Rais Samia kuifungua nchi inakamilika kwa wakati na kwa ufanisi mkubwa," anasema.

Hivyo, anasema ujenzi wa mradi wa barabara hiyo umetumia fedha nyingi, anawataka watumiaji wa barabara hiyo kuhakikisha wanaitunza miundombinu yake ili iweze kudumu na kutumika kwa muda mrefu zaidi kama ilivyotakiwa na kuwa mabalozi wema kwa kuwafichua wizi wa miundombinu ikiwemo taa na alama za barabarani.






# Barabara Tabora-Koga-Mpanda ya kilometa 342.9 yafunguliwa

- **RAIS** Samia asema barabara hiyo ni kichocheo cha uchumi kwa wananchi wa Tabora, Katavi na Rukwa
- **ITAZIDISHA** ushirikiano wa kibiashara baina ya Tanzania na nchi jirani zikiwemo DRC, Burundi na Zambia

**NA HAMIS SHIMYE, SIKONGE**

SHIDA ya zaidi ya miaka 20 sasa imeondoka. Ndivyo unavyoweza sema namna adha kubwa ya usafiri waliyokuwa wanaipata wananchi kutoka mikoa ya Tabora na Mpanda katika kusafirisha bidhaa zao kutoka mkoa mmoja kwenda mwingine kutumia siku nne au hata saa 7 hadi nane sehemu ya saa moja na nusu.

Umbali wa kutoka Sikonge mkoani Tabora hadi Mpanda(Katavi) ni sehemu yenye umbali wa saa moja na nusu hadi mawili lakini kabla ya ujenzi wa barabara ya Tabora-Koga-Mpanda yenye urefu wa kilometa 342.9, hali ilikuwa mbaya ikiwemo vifo, watu kuharibikiwa mazao yao.

Jambo hili lilisababisha serikali kuja na mipango mikakati ya ujenzi wa barabara ya lami katika eneo hilo, ili kuweza kuwaondolea adha kubwa wananchi waliokuwa wanaipata walipokuwa wanaitumia barabara hiyo, ambapo wananchi wanaishukuru serikali na Wakala ya Barabara Tanzania (TANROADS).

> **Najisikia faraja kubwa kukamilika kwa barabara na kuwaondolea adha wananchi waliyokuwa wanaipata kwa kuwa barabara iliyokuwepo haikuwa nzuri, ilikuwa hatari kubwa kwao.**
>
> **RAIS SAMIA SULUHU HASSAN**



Akifungua barabara hiyo, Rais Samia Suluhu Hassan anasema anajisikia faraja kubwa kukamilika kwa barabara na kuwaondolea adha wananchi waliyokuwa wanaipata kwa kuwa barabara iliyokuwepo haikuwa nzuri, ilikuwa hatari kubwa kwao.

Anasema kufunguliwa kwa barabara hiyo ni kichocheo kikubwa cha uchumi kwa wananchi wa Tabora na Mpanda ambao wengi wao ni wafugaji na wakulima, sasa wataweza kufanya shughuli zao kwa ufanisi mkubwa ndani ya mikoa hiyo na mingineko pamoja na nchi jirani.

"Nia na malengo ya serikali ni kufanya ujenzi wa miradi ya barabara, ambapo nawaahidi leo nimeifungua barabara ya Tabora-Koga-Mpanda yenye urefu wa kilometa 342.9, serikali pia ina mpango wa ujenzi wa barabara ya Kwagwira hadi Bandari ya Kalema mkoani Katavi ndani ya mwaka ujao wa fedha" anasema.

Barabara ya Tabora,



# Barabara ya Tabora-Koga-Mpanda yafunguliwa

Koga-Mpanda yenye urefu wa kilometa 349 iliyogharamiwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AFDB) kwa gharama ya sh. bilioni 473.45, ikiwa ni mkopo wenye masharti nafuu, Rais Samia anasema itakuwa na mchango mkubwa kwa nchi kukuza uchumi na kuifungua mikoa ya Katavi na Tabora.

Rais Samia anasema ujenzi wa barabara za lami mkoani Tabora, umekuwa na mafanikio makubwa na umesaidia kuufungua mkoa wa Tabora na Katavi na kurahisisha maendeleo kwa wananchi wa maeneo hayo, ambao awali walikuwa wanapata shida na adha kubwa ya usafiri.

"Nafurahi sana kuwepo hapa na kuifungua barabara hii. Hii ni ishara kubwa kuwa mkoa unafunguka na kukua kiuchumi na barabara hii ina umuhimu mkubwa kwa kuwa inakwenda kuufungua mkoa wa Tabora na Katavi na nchi za jirani," anasema.

Anaongeza:"Nawashukuru sana AFDB kwa ushirikiano wao wanaoendelea kutupa na kufanikisha ujenzi huu na miradi mingine, wamekuwa watu safi kwetu na wamedhihirisha kweli wao ni Benki ya Maendeleo Afrika. Hiki walichokifanya kwa Tanzania kina thamani kubwa."

Anasema ana matumaini makubwa kumalizika kwa barabara hiyo sasa wakulima wa mahindi, wafugaji wa nyuki watasafirisha bidhaa zao kwa kuwa ujenzi wa barabara hiyo umewaondolea adha kubwa waliyokuwa nayo awali ya kutokuwepo kwa usafiri wa uhakika.

"Sasa mwananchi wa Tabora wataweza kwenda Katavi, Burundi au DRC kufanya biashara. Barabara hii ni muhimu kwa kuwa imerahisisha usafiri kwa wananchi. Tunapaswa kuitunza iweze kudumu kwa kuwa barabara hii ni kichocheo cha uchumi, utalii," anasema.

Rais Samia anasema pia, barabara hiyo ina umuhimu kwa wananchi wa mikoa ya Tabora, Katavi na Rukwa na nchi za jirani, ikiwemo Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), Zambia ambao wamekuwa wakifanya shughuli mbalimbali za kibiashara na Tanzania.

"Nawaahidi katika mwaka ujao wa fedha tutajenga barabara ya Mpanda hadi Kalema. Lengo la ujenzi huo ni kurahisisha ufanyaji wa biashara wa mizigo kutoka Bandari ya Dar es Salaam, Kalema hadi DRC. Hii lazima tuijenge kwa kuwa ni barabara muhimu" anasema

Anaongeza : "Nawapongeza sana TANROADS, Waziri kwa kazi kubwa mliyoifanya hadi kufanikisha ujenzi wa barabara hii muhimu, ambayo sasa ile shida kubwa waliyokuwa wanaipata wananchi imekwisha. Sasa ni wakati wa kuitumia barabara hiyo kuvutia wawekezaji na kuhamasisha kilimo na uzalishaji wa asali ili kukuza uchumi wa wananchi wa mikoa ya Ukanda wa Magharibi," anasema Rais Samia.

**"Mwaka ujao wa fedha kuna miradi mingi ya barabara itatekelezwa ikiwemo ujenzi wa barabara kutoka Sikonge hadi Mbeya na nyinginezo ambazo zitakwenda kufungua uchumi wa nchi na maeneo husika ya watu. Rais Samia amedhamiria kuijenga nchi" anasema Anasema anampongeza Rais Samia kwa kazi kubwa anayoifanya ya ujenzi wa miundombinu maeneo mbalimbali ya nchi, hivyo akiwa kama msaidizi wake atahakikisha miradi yote inamalizika kwa wakati na kwa kiwango kinachotakiwa.**

## AWAPA KARIPIO WEZI MBIUNDOMBINU YA BARABARA, AVIPA MAAGIZO VYOMBO VYA ULINZI NA USALAMA

Anasema serikali inajitahidi kufanya ujenzi wa miradi ya barabara, madaraja maeneo mbalimbali ya nchi, lakini kumekuwepo na watu wanaohujumu miradi hiyo, hivyo sasa ni wakati wa kuwachukulia hatua kwa kuwa wanaofanya vitendo hivyo ni wahujumu wa uchumi.

"Nina taarifa kuna watu wameiba taa na alama za barabarani, naviomba vyombo vya ulinzi na usalama kuwachukulia hatua. Miradi hii na mingine yote ya barabara ni yetu na tunapaswa kuilinda kwa nguvu kubwa," anasema.

Rais Samia anasema kuna umuhimu mkubwa wa Watanzania kutunza na kulinda miundombinu ya barabara na madaraja ili idumu kwa muda mrefu na wote watakaohusika na vitendo vya uhujumu miundombinu hiyo wachukuliwe hatua za kisheria.

"Tunzeni miundombinu kwa manufaa yenu wenyewe kumbukeni maendeleo ni safari na kila safari huanza na hatua za awali," anasisitiza Rais Samia.

## WAZIRI PROFESA MBARAWA ATAJA MIPANGO YA RAIS SAMIA UJENZI WA BARABARA

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa anasema Serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Samia imepanga kuunganisha barabara ya Kagwila - Karema ili kuvutiwa wasafirishaji wa kwenda DRC kutumia njia hiyo hali itakayochochea maendeleo ya mikoa ya Kanda ya Magharibi.

Anasema serikali pia ina mpango wa kujenga barabara za Ipole - Rungwa na Mpanda-Uvinza kwa kiwango cha lami ili kukuza fursa za kilimo, mifugo, utaliii katika Hifadhi ya Katavi na biashara kati ya Tanzania na nchi za DRC, Rwanda, Burundi na Zambia na hivyo kukuza Uchumi.

"Nia na malengo ya serikali ya awamu ya sita ni makubwa, hivyo akiwa kama Waziri atahakikisha anasimamia mipango hiyo ili serikali iweze kutekeleza kwa kasi kubwa kwa kuwa ina dhamira kubwa ya kuwaondolea shida wananchi wa maeneo hayo," anasema.

Anasema ujenzi wa barabara hiyo ni faida kubwa kwa nchi, huku akiwaahidi wananchi serikali itaendelea ujenzi wa miradi mbalimbali ya barabara kwa kuwa dhamira ni kuhakikisha nchi inakuwa na barabara za lami ili kurahisisha usafiri na usafirishaji.

"Mwaka ujao wa fedha kuna miradi mingi ya barabara itatekelezwa ikiwemo ujenzi wa barabara kutoka Sikonge hadi Mbeya na nyinginezo ambazo zitakwenda kufungua uchumi wa nchi na maeneo husika ya watu. Rais Samia amedhamiria kuijenga nchi," anasema.

Anasema anampongeza Rais Samia kwa kazi kubwa anayoifanya ya ujenzi



# Barabara ya Tabora-Koga-Mpanda

wa miundombinu maeneo mbalimbali ya nchi, hivyo akiwa kama msaidizi wake atahakikisha miradi yote inamalizika kwa wakati na kwa kiwango kinachotakiwa.

**AFDB YAIPONGEZA SERIKALI KUTATUA SHIDA**

Meneja Mkazi wa Benki ya Maendeleo ya Afrika nchini Tanzania, Dk. Patricia Laverley, anasema kukamilika kwa barabara hiyo historia kwao kutokana na shida waliyokuwa wanaipata wananchi wa mikoa ya Katavi na Tabora hadi wao wakaamua kutoa mkopo kwa serikali.

"Wananchi walikuwa wanapata shida sana katika usafiri hususan eneo la Mto Koga, awali hali imekuwa kutokana na uwepo wa barabara nzuri na ujenzi wa daraja katika eneo hilo, ambapo awali hali ilikuwa mbaya na watu walishindwa kufanya shughuli zao za kiuchumi," anasema.

Anasema ujenzi wa barabara hiyo ni faraja kubwa kwao kwa kuwa jambo walilolianza 2019 kwa kuweka jiwe la msingi mkoani Katavi sasa limekamilika ikiwemo Rais Samia kufungua barabara hiyo, ambayo ni mkombozi kwa uchumi wa wananchi wa maeneo hayo na nchi jirani.

"Natoa salamu za dhati kutoka AFDB kwako Rais Samia kwa kazi kubwa ya ujenzi wa barabara hii, kwa kuwa wananchi wa Tabora na Katavi wamepata ahueni kubwa na kuimarisha uchumi wa wananchi. Awali hali ilikuwa mbaya ikiwemo watu kutumia muda mwingi wakiwa barabarani," anasema.

**RC DKT. BATILDA ASEMA SIKONGE SASA KAMA ULAYA**

Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Balozi Dkt. Batilda Burian anasema ujenzi wa barabara hiyo umesaidia kuibadilisha Tabora na wilaya ya Sikonge, ambapo uwepo wa taa umeifanya eneo hilo kuwa kama Ulaya kutokana na ubora na upekee uliopo sasa kutokana na barabara hiyo.

"Tunakupongeza Rais Samia kwa barabara hii, imeifanya Sikonge kuwa kama Ulaya, imesaidia wakulima kufanya shughuli zao na hata kuwa na uhakika wa biashara zao kwenda maeneo mbalimbali kwa kuwa kuna biashara nzuri na ya kisasa," anasema.

**RC KATAVI AIPONGEZA SERIKALI KWA BARABARA HIYO**

Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mwamvua Mrindoko, anasema ujenzi wa barabara hiyo umesaidia kuufungua mkoa wao ikiwemo wananchi wanaofanya shughuli zao za Kilimo kufanya biashara zao



**"Hii ni historia kwetu, uwepo wa barabara hii sasa wakulima, wafugaji wa nyuki wanafanya shughuli zao bila wasiwasi na kwa usalama mkubwa kwa kuwa kuna barabara nzuri na yenye viwango imejengwa na serikali,"**

**Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mwamvua Mrindoko**



bila usumbufu na kukuza uchumi wa mkoa.

"Hii ni historia kwetu, uwepo wa barabara hii sasa wakulima, wafugaji wa nyuki wanafanya shughuli zao bila wasiwasi na kwa usalama mkubwa kwa kuwa kuna barabara nzuri na yenye viwango imejengwa na serikali," anasema.

**BUNGE LAPONGEZA HUKU MWENYEKITI KAKOSO AKIELEZA HISTORIA YA USUMBUFU WALIOKUWA WANAUPATA KATIKA BARABARA HIYO.**

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, Moshi Kakoso, ambaye pia ni Mbunge wa Mpanda, anasema barabara hiyo ina historia kubwa kwake ikiwemo usumbufu mkubwa aliokuwa anaupata pamoja na wananchi kutoka Katavi kwenda Tabora.

"Miaka 20 nyuma hali ilikuwa mbaya sana nina historia nako, ujenzi wa barabara hii sasa umesaidia hata kupandisha gunia la mahindi ambapo limefika elfu 50 kutoka elfu 18 kipindi cha nyuma. Nakupongeza sana Rais Samia nakumbuka mengi sana kuhusiana na shida iliyokuwepo eneo hilo," anasema.

Anasema akiwa mbunge kutoka mkoa wa Katavi na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, anampongeza Rais Samia kwa ujenzi wa miradi mbalimbali ya barabara ambayo imekuwa chachu ya mafanikio kwa kurahisisha usafiri na usafirishaji.

**MBUNGE SIKONGE, WANANCHI WASHEHEREKEA**

Mbunge wa Sikonge, Joseph Kakunda anasema anaipongeza serikali kwa ujenzi wa barabara hiyo kwa kuwa imerahisisha usafiri kwa wananchi wa maeneo hayo na Katavi ambao walikuwa wanapata shida kubwa na wanaishukuru serikali ya awamu ya sita kwa kusema ahsante sana.

"Tunakushukuru Rais Samia na ahsante sana kwa barabara hii, umekuwa mkombozi wetu kwa kuwa umefanya kazi kubwa ya ujenzi wa barabara hii, ambayo kwetu ni maisha na uchumi kwa sababu imerahisisha usafiri wa wananchi kutoka Tabora kwenda Mpanda" anasema.

Naye, Khamisi Kabwalibwali mkazi wa Tutuo, Tabora alisema akiwa kama mkazi na mwenyeji wa Tabora kwa zaidi ya miaka 48, Rais Samia amekuwa kiongozi wa mfano katika maendeleo, ambapo serikali yake imeweza kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kwa kasi kubwa.

"Nilikuwa napata kipindi cha nyuma kusafirisha mazao kupeleka Mpanda. Rais Samia amefanya makubwa sana na hili la barabara ya Tabora kwenda Mpanda. Mungu amlinde aisee ametuokoa maana hali ilikuwa mbaya sana nyakati za mvua, ambapo tulikuwa tunapata shida kubwa kutokana na adha ya usafiri," anasema.

Hivyo, anasema anampongeza Rais Samia kwa ujenzi wa barabara hiyo kwa kuwa imekuwa na faida kubwa kwao ikiwemo usafirishaji wa mazao na shughuli nyingine wanazofanya sasa kuwa na faida kubwa na wanatumia muda mchache kutoka Tutuo kwenda Mpanda.



# TANROADS yaelezea ubora wa barabara ya Tabora – Koga – Mpanda

■ **MTENDAJI** Mkuu Eng. Mativila asema imesanifiwa kubeba magari yenye uzito tani 65




**RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan, akizungumza na viongozi mbalimbali pamoja na wananchi katika sherehe za ufunguzi wa barabara ya Tabora-Koga-Mpanda 342.9 km zilizofanyika Sikonge mkoani Tabora.**

**NA MWANDISHI WETU**

WAKALA ya Barabara Tanzania (TANROADS) imeitaja barabara ya Tabora-Koga-Mpanda ni moja ya barabara bora zilizojengwa na zinazoendelea kujengwa nchini zenye uwezo kupitisha magari yenye uzito wa tani 65 na ujenzi wake umegharimu sh. bilioni 473.95.

Mtendaji Mkuu wa TANROADS, Eng. Rogatus Mativila, anasema barabara hiyo ina urefu wa kilometa 342.9, ambayo imejengwa kwa kiwango cha lami na kampuni tatu za ujenzi ili kufupisha muda wa ujenzi wa mradi huo, ambao ni muhimu kwa maendeleo ya wananchi wa mikoa ya Tabora na Katavi.

Anasema mradi wa ujenzi wa barabara hiyo, umesaidia kuondoa adha kubwa waliyokuwa wanakumbana nayo wananchi kipindi cha mvua, ambapo walikuwa wanalala njiani kwa siku mbili, ambapo barabara hiyo imejengwa kwa teknolojia ya kisasa na viwango vya kimataifa.

Eng. Mativila anasema mradi wa ujenzi wa barabara ya Tabora (Usesula) - Koga - Mpanda yenye urefu wa kilometa 342.9 kwa kiwango cha lami ni mradi uliokuwa na umuhimu mkubwa kwa maendeleo ya nchi kutokana na barabara hiyo kuunganisha mikoa ya Tabora, Mpanda na Rukwa kwa lami.

"Barabara ya Tabora – Koga – Mpanda yenye urefu wa kilometa 342.9 ni Barabara kuu inayounganisha Mkoa wa Katavi na Mkoa wa Tabora. Barabara hii ilikuwa ikipitika kwa shida sana kipindi cha mvua hasa katika maeneo ya Mto Koga kutokana na mafuriko ya maji ya mvua" anasema.

Aidha, anasema kutokana na umbali mrefu, usafiri kati ya Mpanda na Tabora ulikuwa ukichukua takriban saa saba (7) hadi zaidi ya siku mbili kipindi cha mvua. Hali hii ilisababisha adha kubwa kwa wasafiri na wasafirishaji wa bidhaa mbalimbali.

"Ili kuondoa adha hii Serikali ilifanya kila jitihadi ya kupata fedha za ujenzi wa Barabara hii kwa kiwango cha lami na hatimaye Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) , ilikubali kutoa Mkopo wa Masharti nafuu kwa ajili ya ujenzi wa mradi huu," anasema.

Kwa mujibu wa Eng. Mativila, AfDB kwa kushirikiana na Tanzania kupitia Programu ya "Transport Sector Support Program (TSSP)," walikubaliana kuanza ujenzi wa mradi huo, ambao umemalizika na Rais Samia kuufungua na kuwa mmoja wa miradi yenye manufaa makubwa kwa nchi.



**BARABARA hiyo imejengwa kwa sh. bilioni 473. 95, ambapo gharama halisi zilizotumika katika Ujenzi (Works Contract) ni Shilingi 450,992,680,059.98, Usimamizi (Supervision Services) Shilingi 19,685,118,410.00, Usanifu Shilingi 1,433,638,166.00 na Shilingi 1,846,109,058.33**

**Mtendaji Mkuu wa TANROADS, Eng. Rogatus Mativila,**

Anasema barabara hiyo imejengwa kwa sh. bilioni 473. 95, ambapo gharama halisi zilizotumika katika Ujenzi (Works Contract) ni Shilingi 450,992,680,059.98, Usimamizi (Supervision Services) Shilingi 19,685,118,410.00, Usanifu Shilingi 1,433,638,166.00 na Shilingi 1,846,109,058.33 kwa ajili ya Fidia kwa watu walio athiriwa na Mradi kwa mujibu wa sheria.

Kulingana na usanifu, Eng. Mativila anasema barabara hiyo imejengwa kwa viwango ikiwemo upana wa Barabara (Carriage way) ni mita 6.5 na mabega (Shoulders) upana wa mita 1.5 kila upande, ambapo imeifanya barabara hiyo kuwa imara na yenye ubora.

"Mitaro ya maji ya mvua na makalavati yamejengwa kuondoa maji katika eneo la barabara. Hii ni pamoja na ujenzi wa Daraja la urefu wa mita 120 kwenye mto Koga. Daraja ambalo limejengwa kwa ufanisi mkubwa kuwezesha kudumu kwa muda mrefu," anasema.

Pia, Eng. Mativila anasema matabaka (Pavement layers) ya Barabara hii yamejengwa kwa kiwango kikubwa, ikiwemo tabaka la kwanza ni Tuta lililojengwa kwa udongo wenye uimara wa G3, 7 na 15 kwa unene wa milimita 150 kwa kila tabaka;

"Tabaka la msingi wa chini (Sub base) lenye unene wa milimita 200 lililojengwa kwa kuchanganya changarawe na saruji (C1); Tabaka kuu la msingi (base course) lenye unene wa milimita 150 lililojengwa kwa mawe yaliyosagwa kwa vipimo maalumu (CRR) na;Tabaka la juu (lenye lami ngumu) unene wa milimita 50," anasema.

Eng. Mativila anasema ili kufupisha muda wa ujenzi, mradi uligawanywa katika sehemu tatu ambazo sehemu ya kwanza ni Usesula-Komanga (km 108) na barabara unganishi za mji wa Sikonge (km 9.6), ambapo mkandarasi alipewa kujenga eneo hilo.

Anasema mkandarasi aliyejenga sehemu ya kwanza ni Kampuni ya Jiangxi Geo - Engineering (Group) Corporation Ltd kutoka China kwa gharama ya Shilingi 165,219,050,413.09 pamoja na VAT na ujenzi ulikamilika Oktoba 25, 2021.

"Kampuni iliyosimamia ujenzi wa sehemu ya kwanza ni LEA International Ltd JV LASA kutoka Canada, ikishirikiana na Advance Engineering Solutions ya Tanzania kwa gharama ya dola za Marekani USD 2,818,363.48 ambayo ni sawa na Shilingi 6,482,236,004.00,'' anasema.

Anasema sehemu ya Pili ni Komanga - Kasinde (km 108) na barabara unganishi ya mji wa Inyonga (km 4.8), ambapo mkandarasi aliyejenga sehemu hiyo ni Kampuni ya China Wu Yi Co. Ltd kwa gharama ya Shilingi 151,969,801,249.68 pamoja na VAT. Ujenzi ulikamilika Oktoba 18, 2021.

Kampuni iliyosimamia ujenzi wa sehemu hii ni Egis Intaernational Ltd kutoka Ufaransa kwa gharama ya Euro 698,815.77 na dola za Marekani USD 2,350,332.47, ambayo ni sawa na shilingi 7,152,804,106.00 hadi ujenzi ulipokamilika.

Anasema sehemu ya Tatu ni Kasinde-Mpanda (km 105.389) na barabara unganishi ya kijiji cha Uruwira (km 2.3), ambapo mkandarasi aliyejenga sehemu hiyo ni Kampuni ya China Railway Seventh Group Co. Ltd kutoka China kwa gharama ya Shilingi 133,803,828,397.29 pamoja na VAT na ujenzi ulikamilika Desemba 26, 2021.

Anasema mhandisi mshauri aliyesimamia ujenzi wa sehemu hii ya tatu ni Kampuni ya Afrisa Ltd ya Tanzania ikishirikiana na Kampuni ya Dasan Ltd kutoka Korea ya Kusini kwa gharama dola za Marekani USD 2,624,561.00 na Shilingi 13,588,000.00, ambazo ni sawa na jumla ya Shilingi 6,050,078,300.

Hivyo, anasema kukamilika kwa mradi huo kumekuwa na faida kubwa, huku akiwataka wananchi kuulinda mradi huo dhidi ya wizi na uharibifu wa miundombinu ya barabara, hususan taa za barabarani, ambapo kumeanza kujitokeza matukio mbalimbali ya wizi katika mradi huo.

# BARABARA YA NYAHUA -CHAYA KILOMITA 85.4 NA KOGA - MPANDA KILOMITA 342.9 MKOANI TABORA. KABLA NA BAADA YA UJENZI



















TANROADS
Tanzania National Roads Agency
Good roads for national development

# BARABARA YA NYAHUA -CHAYA KILOMITA 85.4 NA KOGA - MPANDA KILOMITA 342.9 MKOANI TABORA. KABLA NA BAADA YA UJENZI








